

Vidokezo vya Kuendesha Gari kwa Usalama Majira ya Baridi

Zuia ajali, majeraha na usumbufu



Peleka gari kwa fundi magari afanye ukaguzi wa matengenezo:

Kagua tredi za magurudumu. Magurudumu ya kuendeshwa thelujini huongeza uwezo wa kusimama na yanaweza kuzuia ajali.

Kagua injini na viowevu vyote.

Dumisha viwango sahihi vya maji ya kuosha vioo, rediata na mafuta kwenye tenki.

Jitayarishe - Huchukua muda zaidi/anza mapema:

Soma habari za eneo lako (wktv.com) upate taarifa za hali ya hewa/kufungwa kwa barabara na ripoti za hali za barabara <https://511ny.org/>

Kabla ya kuendesha gari - ondoa theluji kwenye bomba la moshi, washa gari lipate joto, ondoa theluji kwenye madirisha, umbo la gari na taa.

Kumbuka kuwa majukwaa na madaraja huganda kwa baridi kabla ya barabara

Hakikisha kuna nafasi kubwa kati ya gari lako na unalolifuata

Punguza kasi ya gari lako; theluji na barafu huwa telezi. Kusimama huchukua muda zaidi

Kuwa stadi wa kudhibiti gari lako baada ya kuteleza; barabara huwa telezi majira ya baridi

Fahamu kama una Mfumo wa Breki wa Kuzuia Kufungana kwa Magurudumu (ABS); USIWAHI kupiga pampu breki za ABS

Beba vifaa vya dharura:

Tochi, kofia, glavu, blanketi na kurunzi (viberiti katika mfuko usiopenyeza maji)

Maji ya kunywa; njugu, matunda yaliyokaushwa na peremende

Beleshi, kifaa cha kuondoa theluji na nyaya za kuwasha gari kwa betri la gari jingine.

Changarawe, chumvi/kiyeyushaji barafu au vibanzi vya mbao vya kukusaidia ukikwama na kulipa gari lako uwezo wa kujikwamua

TS. Kiswahili. Winter Safe Driving Tips. 2020

